Ombi la Kurekebisha Bei za Majisafi na Majitaka la

MAMLAKA YA MAJISAFI NA MAJITAKA KIGOMA (KUWASA)

Utangulizi

1. Tarehe 17 Mei 2011, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji ("EWURA") ilipokea ombi kutoka KUWASA kuhusu yafuatayo:

(a) kuongeza bei ya sasa ya maji kwa wateja wenye dira kwa kiwango cha kati ya asilimia 100 na 433;

(b) kuongeza bei ya sasa ya maji kwa wateja wasio na dira kwa kiwango cha kati ya asilimia 233 na 2,200;

(c) kuongeza kodi ya dira kwa asilimia 66.67 kutoka TZS 300 hadi TZS 500 kwa mwezi;

(d) kuongeza ada ya maunganisho mapya ya maji kwa kiwango cha kati ya asilimia 75 na 100;

(e) kuongeza ada ya kurejesha maji baada ya kukatiwa kwa kiwango cha kati ya asilimia 200 na 400;

(f) kuanzisha tozo ya huduma ya kati ya TZS 1,000 kwa mwezi hadi TZS 5,000 kwa mwezi;

(g) kuanzisha amana ya dira ya TZS 150,000 kwa kila unganisho jipya; na

(h) kupendekeza kuwa bei na tozo hizo kama zitapitishwa zianze kutumika rasmi tarehe 1 Julai 2011.

Ushirikishwaji wa Wadau

2. Kwa mujibu wa kifungu cha 19(2)(h) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Sura ya 414, EWURA ilifanya taftishi kuhusu uhalali wa ombi la kurekebisha bei na tozo zilizopendekezwa. Taftishi hiyo ilihusisha tathmini ya masuala ya kiuchumi na ya kiufundi pamoja na kufanya mkutano wa taftishi tarehe 8 Septemba 2011 katika Manispaa ya Kigoma/Ujiji ili kusikia maoni ya wadau.

3. Wakati wa taftishi, wadau wakiwemo, wananchi, Baraza la Ushauri la Serikali (*Government Consultative Council* ("GCC")), na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma zinazodhibitiwa na

EWURA (*Consumers Consultative Council* ("EWURA CCC")) walipata fursa ya kuchunguza na kutoa maoni yao kuhusiana na uhalali wa ombi hilo la KUWASA. KUWASA vilevile ilipewa fursa ya kujibu moja kwa moja hoja za wadau kwenye mkutano huo na pia kwa kuwasilisha EWURA majibu ya hoja za wadau kwa maandishi.

4. EWURA CCC walihoji, pamoja na mambo mengine, bei kubwa ya maji kulinganisha na Mamlaka nyingine za maji zilizopo katika kanda ya Ziwa; kuwepo kwa bei tofauti kati ya wateja wa majumbani ambao ni raia na wale wasio raia; ada kubwa ya maunganisho mapya ya maji; ufanisi duni wa kiutendaji; na ongezeko kubwa katika gharama za utumishi na ukarabati kwa mwaka 2011/12.

5. GCC walihoji, pamoja na mambo mengine, madeni makubwa ya umeme; ukosefu wa huduma za majitaka; ufanisi duni wa kukusanya mapato; upotevu mkubwa wa maji; ukosefu wa mapitio ya mara kwa mara ya bei za maji kulikopelekea KUWASA aombe nyongeza ya kubwa ya bei ya maji kwa mara moja; na gharama kubwa na zisizothibitishwa za rasilmali za Mamlaka zilizopelekea kuwepo na mapendekezo makubwa za uchakavu wa mitambo.

6. Wananchi walihoji kuhusu ongezeko kubwa la bei ya maji, na kwamba ongezeko hilo lilianza kutumika hata kabla KUWASA haijawasilisha EWURA maombi yake kwa kupitishwa; wigo mdogo wa utoaji wa huduma; na tatizo la upungufu wa maji linaloambatana na ratiba isiyofuatwa vizuri ya mgao wa maji.

7. Wakati wa kuhitimisha taftishi tarehe 22 Septemba 2011, KUWASA iliweza kujibu hoja za wadau kwa kiasi cha kuridhisha, na EWURA ilipokea maoni ya kutosha kuweza kufanya maamuzi. Wakati wa uchambuzi wa ombi, KUWASA ilitakiwa, na ilitoa maelezo ya ziada kuhusu ombi lao.

Uchambuzi na marekebisho

8. Kufuatia kukamilika kwa mchakato wa taftishi na uchambuzi, EWURA imefikia uamuzi kwamba ombi la nyongeza ya bei lina mantiki na ni halali isipokuwa:

(a) Makisio makubwa ya gharama za uendeshaji na matengenezo (O&M) kwa mwaka 2011/12 yanayojumuisha

i. makisio makubwa ya gharama za umeme katika uzalishaji maji zilizotokana na makosa ya kimahesabu ambazo zilirekebishwa;

ii. gharama kubwa za usambazaji zilizotokana na makisio makubwa ya gharama za kufunga dira za takriban TZS 525 milioni kwa mwaka. Gharama hizi zilirekebishwa kwa kuzingatia gharama za wastani za kufunga dira moja ambayo ni TZS 20,000 na idadi ya dira 2,000 zilizopangwa kufungwa katika mwaka wa fedha wa 2011/12;

iii. gharama kubwa za ukarabati na matengenezo zilizorekebishwa kwa kuzingati matumizi makubwa ya kasma hiyo katika mwaka wa 2009/10 za kiasi cha TZS 687,866,785 ambazo ziliboresha mtandao na kupunguza ulazima wa kufanya ukarabati na matengenezo makubwa kwa kipindi kifupi kijacho, na

iv. gharama za utumishi ambazo zilirekebishwa kwa kuzilinganisha na Mamlaka nyingine za maji za Daraja B; na

(b) makisio makubwa ya upotevu wa maji ambayo yalirekebishwa kutoka asilimia 35 hadi 30 ili kuendana na mafanikio ya sasa yaliyofikiwa ya kuzuia upotevu wa maji.

9. Maombi na marekebisho ya mahitaji ya mapato ya KUWASA ni kama inavyoonyeshwa kwenye Jedwali hapa chini.

Maamuzi

Jedwali 1: Mahitaji ya Mapato

	Mapendekezo ya Mapato, 2011/12	**Mapato Yaliyoidhinishwa, 2011/12**
	TZS	**TZS**
GHARAMA ZA UENDESHAJI NA MATENGENEZO		
Gharama za Uzalishaji	950,977,320	602,716,280
Gharama za Usambazaji	871,023,720	337,523,720
Gharama za Ukarabati na Matengenezo	359,200,000	98,760,000
Gharama za Utawala	577,416,144	410,765,005
Gharama za Utumishi	1,013,957,360	444,000,000
Gharama za Fedha	14,400,000	6,000,000
Gharama za Matukio na Michango	36,280,000	26,200,000
Gharama za Mahusiano na matangazo	24,400,000	24,400,000
JUMLA NDOGO	**3,847,654,544**	**1,977,865,005**
GHARAMA ZA UWEKEZAJI		
Uchakavu wa Mitambo	248,706,904	248,706,904
Kuchangia Uwekezaji	198,263,010	198,263,010
JUMLA NDOGO	**446,969,914**	**446,969,914**
JUMLA KUU	**4,294,624,458**	**2,424,834,919**

10. Katika kikao chake cha tarehe 16 Desemba 2011, Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA ilijadili ombi la KUWASA na kutoa maamuzi kama inavyoonyeshwa kwenye Agizo hapa chini:

SHERIA YA MAJISAFI NA MAJITAKA

(SURA NA 272)

AGIZO Na. 11-19

(Imetolewa kwa mujibu wa Kifungu Na.28 (d)cha Sheria ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, 2009)

MAMLAKA YA MAJISAFI NA MAJITAKA KIGOMA ("KUWASA"), AGIZO LA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI, 2011

Kichwa cha Agizo

1. Agizo hili litajulikana kama, Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Kigoma ("KUWASA"), Agizo la Kurekebisha Bei za Huduma ya Maji, 2011 na litaanza kutekelezwa kuanzia tarehe 1 Januari, 2012.

Marekebisho ya Bei

2. Bei za maji za Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Kigoma ("KUWASA") zinarekebishwa kulingana na majedwali yaliyopo katika Agizo hili.

Masharti

3. Bei zilizopitishwa zitaambatana na masharti yafuatayo:

(a) Ifikapo tarehe 30 Machi 2012 au kabla ya hapo, KUWASA itawasilisha EWURA mpango wake wa:

(i). kuongeza kiwango cha ufanisi wa ukusanyaji mapato kutoka asilimia 80.7 cha sasa hadi kufikia asilimia 90 ifikapo mwezi Juni 2012;

(ii). kupunguza kiwango cha upotevu wa maji kutoka asilimia 35 cha sasa hadi kufikia asilimia 30 ifikapo mwezi Juni 2012; na

(iii). kulipa madeni yote ya umeme;

(b) ifikapo tarehe 30 Machi 2012 au kabla ya hapo, KUWASA inatakiwa kununua na kufunga dira za maji 2,000 kwa wateja wake wa majumbani;

(c) ifikapo tarehe 30 Aprili 2012 au kabla ya hapo, KUWASA inatakiwa kununua mashine mpya ya kusukuma maji yenye uwezo wa kusukuma mita 250 za ujazo kwa saa;

(d) ifikapo tarehe 30 Juni 2012 au kabla ya hapo, KUWASA inatakiwa kuongeza mtandao wake wa huduma ya maji kwa kuongeza mtandao wa usambazaji maji kutoka eneo

la Vamia hadi Mji mpya (kwa umbali wa kilomita 4) na kutoka eneo la Mlole hadi Gungu (kwa umbali wa kilomita 4);

(e) ifikapo tarehe 30 Juni 2012 au kabla ya hapo, KUWASA inatakiwa kuwasilisha EWURA mpango/makakati wake wa kina wa kuwatambua wateja wasio na uwezo wa kulipia maji kwa minajili ya kuwapa huduma hiyo bure kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Maji;

(f) ifikapo tarehe 30 Juni 2012 au kabla, KUWASA inatakiwa iwe imewasilisha EWURA taarifa ya maendeleo ya utekelezaji wa mpango wa kuimarisha mahusiano, mawasiliano, utoaji habari na uelimishaji wa wateja (customer outreach). Taarifa ya utekelezaji wa mpango huo iwasilishwe EWURA katika maombi yote yajayo ya kurekebisha bei za huduma hiyo. EWURA itazingatia taarifa hiyo wakati wa kufanya tathmini ya uhalali wa maombi husika; na

(g) KUWASA itaendelea kuwasilisha kwa EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa mwongozo wa EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa KUWASA ikilinganishwa na vyombo vingine vya utoaji wa huduma za maji na uboreshaji wa huduma zake. EWURA itazingatia tathmini hii katika kufanya maamuzi ya maombi yote yatakayowasilishwa na KUWASA katika siku zijazo.

Utenguzi

4. Bei za Majisafi na Majitaka zinazotumika sasa zilizopangwa mwaka 2004 zinatenguliwa.

KIAMBATANISHO

Jedwali 1: Bei ya Maji ya Sasa na Iliyoidhinishwa (Wateja wenye Dira)

Kundi la Wateja	**Bei ya Sasa (TZS/m^3)**	**Bei Iliyoidhinishwa (TZS/m3)**
Majumbani	300	630
Taasisi	450	940
Biashara	500	980
Viwanda	600	1,020
Magati	250	TZS10/lita 20
Wataalam toka Nje ya Nchi	600	-

Jedwali 2: Bei ya Maji ya Sasa na Iliyoidhinishwa (Wateja wasio na Dira)

Kundi la Wateja	**Kiwango cha Msukumo wa Maji (Pressure Zones)**	**Bei ya Sasa (TZS/ Mwezi)**	**Bei Iliyoidhinishwa (TZS/ Mwezi)**
Majumbani	Kidogo	5,200	15,750
	Cha Kati	6,400	15,750
	Kikubwa	7,500	15,750
Taasisi		10,000	Hakuna Wateja Wasio na Dira
Biashara		15,000	Hakuna Wateja Wasio na Dira
Viwanda		20,000	Hakuna Wateja Wasio na Dira
Wataalam toka Nje ya Nchi		15,000	Kundi hili litakuwa la Wateja wa Majumbani

Jedwali 3: Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Maunganisho Mapya ya Maji

Kundi la Wateja	**Ada ya Sasa (TZS)**	**Ada Iliyoidhinishwa (TZS)**
Majumbani	40,000	Asilimia 20 ya Gharama ya Maunganisho
Taasisi	50,000	Asilimia 20 ya Gharama ya Maunganisho
Biashara	60,000	Asilimia 20 ya Gharama ya Maunganisho
Viwanda	60,000	Asilimia 20 ya Gharama ya Maunganisho
Wataalam toka Nje ya Nchi	60,000	Kundi hili litakuwa la Wateja wa Majumbani

Jedwali 4: Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Kurejesha Huduma ya Maji baada ya Kukatiwa

Kundi la Wateja	Ada ya Sasa (TZS)	Ada Iliyoidhinishwa (TZS)
Majumbani	5,000	10,000
Taasisi	10,000	15,000
Biashara	15,000	15,000
Viwanda	15,000	20,000
Wataalam toka Nje ya Nchi	15,000	Kundi hili litakuwa la Wateja wa Majumbani

Jedwali 5: Kodi ya Dira ya Sasa na Iliyoidhinishwa

Kundi la Wateja	Kodi ya Sasa (TZS/Mwezi)	Kodi Iliyoidhinishwa (TZS/Mwezi)
Wateja Wote	300	500

Jedwali 6: Amana ya Dira ya Sasa na Iliyoidhinishwa

Kundi la Wateja	Amana ya Sasa (TZS/Unganisho)	Amana Iliyoidhinishwa (TZS/Unganisho)
Wateja Wote	-	-

Jedwali 7: Tozo ya Huduma (Service Charge) ya Sasa na Iliyoidhinishwa

Kundi la Wateja	Tozo ya Sasa (TZS/Mwezi)	Tozo Iliyoidhinishwa (TZS/Mwezi)
Majumbani	-	1,500
Taasisi	-	2,200
Biashara	-	2,300
Viwanda	-	3,300
Magati	-	-
Wataalam toka Nje ya Nchi	-	Kundi hili litakuwa la Wateja wa Majumbani

Dar es Salaam HARUNA MASEBU

Mkurugenzi Mkuu

16 Desemba 2011